5. Sambaza Kimaisha

Ni jukumu letu kama kikundi cha maisha kueneza na kushirikiana na wengine makanisani na hata katika jamii zetu, yale yote tunayoyafahamu na yalio umuhimu maishani.

Shiriki na kundi lako

- Shiriki yale umejifunza na wengine kundini.
- Wacha yabadili moyo wako.
- Wakati moyo wako umebadilika, matendo yako pia yatabadilika.
- Watu wengine wataona mabadiliko maishani mwako na watatamani kujua mengi kuhusu Yesu.

Shirikisha jamii yako

- Tazama kwa makini ulipo.
- Ni mahitaji gani yaliyoko katika jamii yako? Kama kikundi mnaweza kuungana na kuhudumia jamii yenu.
- Pamoja kama kikundi mnaweza kuleta mabadiliko katika jamii.

Kundi lako linapaswa kujifunza kuhusu upendo wa Yesu vile vile mnapaswa kuonyeha upendo kwa wale waliowazunguka. Kundi lenu linapaswa kuangalia mahitaji ya jamii yenu na kujaribu kusaidia. Makundi mengine yamepanda mashamba kusaidia masikini wengine wamesaidia wakongwe na mayatima.

Swali.. kundi lenu litafanya nini?

Washirikishe viongozi wengine katika mikutano ya viongozi kuhusu jambo hilo

Viongozi wa makundi katika eneo moja wanakutana na viongozi wa makundi ya maeneo mengine. Mikutano hii huitwa 'Kitawi'.

Kila tunapokutana kama Kitawi, tunaomba pamoja, tunajadiliana kuhusu shida na changamoto zinazotukumba. Tunatiana moyo.

Tunashirikiana kuendeleza kazi ambayo Mungu ametuitia.

6.Makundi ya maisha: Kupandwa Kwao

Makundi haya hayapaswi kubaki yalivyo kwa kipindi kirefu. Tunapokutana, Inapaswa tualike watu wapya kila mara wajiunge nasi. Wakati kundi lako limekutana kwa mda wa kama miezi sita, ni bora kundi lako lijaribu kuzalisha kundi jengine. Mwaweza kupanda makundi mengi mnavyodhamiria.

TAMBUA wale wana uwezo wa kuwa viongozi bora

WAFUNZE jinsi ya kuongoza Kisha **PANDA KUNDI** jipya katika kijiji chako au nyumbani kwako

SAIDIA kundi hilo jipya na kiongozi wao pia

WEZESHA/MWEKE HURU kiongozi mpya na kundi lake wawe kundi huru linalojiendesha kivyake

ALIKA viongozi wapya katika mkutano wa baraza la viongozi kila mwezi.

RUDIENI mambo haya kwa kikundi kipya na katika kikundi chenu baada ya muda.

Anwani yako, simu na barua pepe.

Tuko hapa kukusaidia.
Dignity UK Office: hello@dignityonline.org.uk

Life Group Leaflet, Swahili. © Dignity 2016.
Dignity ni Shirika halali nambari 1122656.
Dignity (Worldwide) ni kampuni ndogo na dhamana,
imesajilliwa katika Uingereza na Wales nambari 6394480.

Vikundi vya Maisha

Ni nini? Na vina fanya kazi vipi?

DIGNITY
MAISHA YA AJABU, MIUJIZA YA KILA SIKU

Vikundi vya Maisha vina husisha watu kutoka machimbuko mbali mbali ambao hukutana sehemu tofauti tofauti, mfano, shuleni , chini ya miti, manyumbani, viwanjani miongoni mwa sehemu zinginezo. Makundi haya hujifunza pamoja kuhusu Yesu na hufanya kazi pamoja kubadili na kuboresha jamii zao.

1. Kila Mmoja ana Nafasi Yake

Kila mmoja anakakaribishwa awe mmoja wa Kundi la maisha, bila kujali yeye ni nani au anafanya nini.

Alika marafiki zako, majirani, watu kutoka makanisa tofauti tofauti ikiwemo wale wasioenda kanisani. Wote wanawezajiunga na kundi la maisha. Yesu aliketi na wenye dhambi licha ya kuwa hakukubaliana na mienendo yao, aliwaonyesha upendo. Kila mmoja anakaribishwa na anapaswa kupokelewa na kutunzwa vyema.

Soma Matendo ya Mitume 2:42-47. Kutaneni mara kwa mara, Jifunzeni, shuhudianeni , Ombeni pamoja vile vile kusaidiana- kama vile kanisa la awali lilivyofanya.

Kiongozi anapaswa kuandaa mkutano wa kundi ila hapaswi kufanya kila kitu. Twaweza jifunza kupitia kila mmoja wetu. Sote twaweza changia. Baada ya muda waweza funza wengine jinsi ya kuandaa mikutano pia.

Vigezo muhimu vya mikutano

1. Andaa mkutano mahali ampapo wote wanaweza fika. Inaweza kuwa nyumbani, chini ya mti, katika kiwanja ama katika shule ya karibu.
2. Kutaneni kila wiki wakati na sehemu hio hio.
3. Mikutano inapswa kuanza na kumalizika kwenye muda ulioratibiwa ili watu waweze kupanga muda uliosalia wa siku yao.

Soma Wakorintho wa kwanza 12:12-31. Sote ni sehemu tofauti ya mwili mmoja na kila mmoja wetu ana jukumu la kutekeleza.

2. Makundi yanayo badilisha Maisha

Uongozi wa kikao kidogo

Kila kikundi kinapewa mwongozo wa kutumia kila wiki. Fuata mwongozo bila kupuuza mijadala, mifano na michezo ya kuigiza iliyoko kenye mwongozo. Kundi lako linahitaji yote haya kujifunza vyema.

Jaribu kutozungumza sana katika mikutano. Mikutano hii si fursa ya kuhubiri. Ruhusu wengine wachangie, tanaweza kujifunza kupitia kwa maoni ya wengine.

Usiruhusu mtu mmoja kuzungumza sana, himiza wengine pia wachangie au kutoa maoni yao. Wahimize wanachama wawe wakweli na wazi katika michango na majibu yao.

Saidia Kundi lako na maarifa ya kutenda yale waliojifunza. Mara kwa mara mwongozo uliopewa utakusaidia na kukupa maarifa.

Mungu anakusudia kutubadilisha

Soma Mathayo 28:19-20. Tunapaswa kuwafanya wengi wawe wafuasi wanao iga na kuishi kama kristo, sio tu wanaoenda kanisani . Mruhusu Roho Mtakatifu abadilishe kundi lenu ili muwe na msukumo/ ari ya kutumikia Jamii yenu.

Shuhudia kuhusu maisha yako kama kiongozi na uwatie moyo wengine wafanye vivyo hivyo.Kuwa mfano mwema kwa maneno na matendo yako. Kiri kwamba nawe pia hufanya makosa wakati mwingine.

Inakupasa ukutane na mwanachama mmoja au wawili wa kundi lako kila wiki. Waonyeshe upendo na uwatie moyo katika kupenda na kumtumikia Mungu katiki kila nyanja ya maisha yao.

Baada ya muda wahimize wengine nao wawatembelee na kuwatumikia wengine pia katikati ya wiki. Waonyeshe upendo na kuwatia moyo kumtumikia mungu kila mmoja kundini anapasawa kutumia kipawa chake.

3. Usaidizi wa Roho Mtakatifu

Roho mtakatifu hutufanya kuwa kama Kristo

Tunakuwa viumbe vipya tunapomfuata Yesu. Tunazaliwa mara ya pili na kuwa wana wa Mungu. Viumbe vipya. Tunapaswa kumuishia Yesu badala ya kujiishia wenyewe.

Soma 2 Wakorintho 5:14-21

Roho Mtakatifu anatusaidia

Mara nyingi ni rahisi kuhisi tumelemewa. Hisia za kutoamini kuwa tunaweza kumudu majukumu yaliyoko mbele yetu. Uongozi wa kundi la maisha linaweza kuwa changamoto na kazi ngumu. Lazima tukumbuke kwamba Mungu ametuma Roho wake Mtakatifu na wale walio katika kundi hili kutusaidia. Tukumbuke kwamba hatuwezi kubadilisha watu, ni kusudi la Mungu kufanya hivyo. Sharti tuwafunze, tuishi nao, na kuwatia moyo, na hayo mengine tuachie Mungu. Hauko peke yako katika kazi hii.

Soma Warumi 8:26-27

4. Jihusishe

Kuwa mkiristo katika kijiji chako ama mtaa wako ina maana ujihusishe. Waweza kupata suluhu na kusaidia katika kutatua matatizo ya watu.

Tumepewa mengi sana na Yesu aliyetuokoa. Uungu ulioko ndani yetu lazima ujitokeze na ujionyeshe kwa wale waliomo kundini na kwa jamii. Wakristo bora hawatambuliki kwa vigezo vya mahubiri ama utajiri. Wao hutambulika kupitia matunda yao. Matunda ni mienendo na maamuzi wanayochukua katika maisha yao.

Soma Luka 6:43-49 na Wagalatia 5:22-23